



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGATANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU TAARIFA YA KIFO CHA MAMA
MJAMZITO MKOANI TANGA

Dodoma; 01.04.2024.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepata taarifa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii juu ya kifo cha Mama mjamzito anayetajwa kwa jina la **Fatuma Musa Suleimani**, kilichotokea alfajiri tarehe 28 Machi, 2024, katika Kituo cha Afya Mikanjuni kilichopo Halmashauri ya Jiji la Tanga mkoani Tanga.

Ofisi ya Msajili wa Baraza inatarajia kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma hizo na endapo watuhumiwa ambao ni wauguzi na wakunga, watabainika kuhusika katika tukio hilo watafikishwa mbele ya Baraza kujibu tuhuma zinazowakabili kwa mujibu wa sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Aidha, Baraza linaendelea kuwakumbusha wauguzi na wakunga wote hapa nchini, kuendelea kutoa huduma kwa kufuata Sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utoaji huduma za Uuguzi na Ukunga ili kuhakikisha jamii inapata huduma iliyo bora na salama.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 (***The Nursing and Midwifery Act, 2010***) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga Nchini ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

Imetolewa na:

Agnes Mtawa
Msajili TNMC